GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA


# Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

**JUZU NO.** 238 **Rajb-Sha'ban** 1445 **AH** **Februari–** 2024 **Tabligh** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

## UFUNUO WA HADHRAT SAYYIDNA AHMAD[as]

### KUHUSIANA NA MWANA ALIYEAHIDIWA[RA]



Hazrat Mirza Ghulam Ahmad of Qadian
The Promised Messiah & Mahdi
(peace be upon him)

"Mimi natunukia juu yako ishara ya rehema Yangu kulingana na kusihi kwako. Na Mimi Nimeheshimu maombi yako kwa ridhaa kwa ajili ya huruma yangu. Na Nimeibariki safari yako. Unaipewa Ishara ya Nguvu, rehema na uhusiano wangu wa karibu. Unajazwa kwa ishara ya uzuri na ukarimu. Na unapewa kifunguo cha ufaulu na ushindi. Amani iwe kwako, Ewe Mshindi. Hivyo ndivyo Mungu Anavyosema, ili wale wanaopenda uhai waokolewe kwa kumatwa kwa kifo, na wale waliozikwa makaburini waweze kutoka. Ili ubora wa dini ya Uislamu na Heshima la Mwenyezi Mungu ijulikane kwa watu. Na pia ukweli uje pamoja na baraka zake zote na uwongo uhame pamoja na madhara yake yote. Ili watu watambue kuwa Mimi ni Mola wa Nguvu na ninafanya nitakavyo. Na ili waamini kuwa Mimi niko pamoja nawe. Na ili wale wasiomwamini Mungu na kukataa Dini Yake na Kitabu Chake na Mtume Wake Mtukufu Mteule Muhammad (s.a.w) amani iwe kwake wakabiliwe na ishara iliyo wazi, na ili njia ya wenye madhambi yadhihirike. Kwa hivyo shangilia, kwamba kijana safi Mwenye umbo mzuri unapewa. Utapokea kijana mwenye akili ambaye atakuwa damu yako na atakuwa katika ukoo wako. Kijana safi na mwenye umbo mzuri atakuja kama mgeni wako. Jina lake ni Emmanuel na Bashir. Amejazwa na Roho Mtakatifu na atakuwa mbali na uchafu wote. Yeye ni Nuru ya Allah. Amebarikiwa ni yule Ajae kutoka mbinguni. Amefuatana na uzuri ambao utakuja pamoja nae. Ataainishwa kwa sifa ya ukuu, ukubwa na utajiri. Atakuja duniani na ataponesha magonjwa mengi ya watu kwa sifa zake za Kimasihi na kwa baraka za Roho Mtakatifu. Yeye ni neno la Allah, kwa kuwa rehema ya Allah na Heshima Lake imemtayarisha na Neno la Utukufu. Atakuwa Mwenye akili zaidi na Mwenye ujuzi, na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa na elimu ya dini na dunia. Atabadilisha tatu kwa nne (maana yake haijaeleweka). Itakuwa jumatatu, jumatatu iliyobarikiwa. Mwana; furaha ya moyo, Mwenye cheo kikubwa, mpole مظهرالاول والاخرمظهرالحق والعلاء كان الله نزل من السماء. Dhihirisho la Mungu wa kwanza na wa mwisho, dhihirisho la Mkweli Aliye juu. Kana kwamba Allah Ameteremka kutoka mbinguni. Ujaji wake utabarikiwa sana na utakuwa msingi wa kuonesha ukuu wa kimbinguni. Tazama! Mwanga uaja, mwanga uliopakwa na Mwenyezi Mungu kwa manukato wa furaha yake. Na Atamwaga Roho yake juu yake na atawekwa chini ya kivuli cha Allah. Atakuwa haraka katika umbo wake na atakuwa namna ya kuwapa uhuru wale waliowekwa katika utumwa. Umaarafu wake utaenea mpaka mwisho wa dunia, na watu watabarikiwa kupitia kwake. Kisha atainuliwa kwa cheo chake cha kiroho katika Peponi. Hiyo ni amri iliyoagizwa tayari. (19:22) "و كان امرا مقضيا



Hazrat Mirza Basheer-ud-Din Mahmood Ahmad Khalifatul Masih II.



Minarat ul Masih Qadian

**Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa..** UK. 8

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

### Ukhalifa Katika Ahmadiyya

Miongoni mwa waahmadiyya khalifa, ni kiongozi wa kiroho mwenye heshima na nafasi maalum. Ni Imani ya waahmadiyya ya kwamba Khalifa nidhihirisho la pili la shani na Jalali ya Allah. Bila shaka Mtume wa Allah anakuja duniani kupanda mbegu, ambayo inaleta duniani wafuasi wenye Imani na ushirikiano thabiti kuhusu yale aliyoyaleta Nabii .Nabii anafanya kazi yake kwa usahihi wa hali yajuu na mafanikio ambayo yanawaacha wapinzani vinywa wazi, Lakini Nabii wa Allah ni binadamu na kama viumbe wengine wa Allah lazima aonje mauti. Hapa ndipo maadui wanapo sherehekea na kuwa na Imani kuwa hapa sasa ndio mwisho wa kazi kubwa aliyoifanya Nabii. Wanakuwa wanahadaika, Allah kwa kupitia mikono safi ya hawa waliotengenezwa na Nabii wanamchagua Khalifa ambaye toka anapo chaguliwa ni Imani ya kila Mwaminio kuwa hilo ni dhihirisho la pili la Allah na Khalifa amechaguliwa na Allah. Mapenzi na heshima wanayokuwanayo kwa Khalifa ni kubwa sana na kila Mwaminio anasubiri kwa hamu na shauku kutekeleza maagizo ya khalifa Mtukufu.

Ukichukua taswira hii kichwani unaweza kupima mwenyewe wito wa Khalifa tul Masih na kutoa Watoto wakatumikie Islam ilivyopokelewa kwa jazba kubwa huku wakiongozwa na agizo la Allah, fastabikuli Khairat. Wazazi walijitokeza kwa wingi ikawa sasa kazi ya kuchuja nani angaliweza kutimiza wajibu huo Barabbara. Huku kulikuwa kujitolea kwa hali yajuu kijana anatoka katika mazingira aliyokulia na anatakiwa kwenda nchi ya mbali, hali ya hewa tofauti, mila, desturi, utamaduni, lugha na chakula. Hayo yote walielezwa na wao neno lao lilikuwa ''tunasikia na kutii''. Mipango ilifanyika wakapewa elimu nzuri na wakatawanywa sehemu mbalimbali za dunia, katika hao waliotayarishwa sisi Afrika Mashariki tukampata Sheikh Mubarak Ahmad ambaye aliweka maskani yake Tabora na akasajili rasmi jumuiya ya Ahmadiyya nchini 1934.

Huzur katutolea wito kuhakikisha kuwa tunatimiza haki za Allah na viumbe wake. kuhakikisha tunasikiliza kwa makini hotuba zake za Ijumaa na vipindi vinavyorushwa na kituo chetu cha MTA. Inakuwaje Mwalimu yupo darasani na mwanafunzi haonekani? Tunamuomba Allah katika mwaka huu 2024 na ijayo tutekeleze maagizo ya Khalifa wa Allah kwa unyenyekevu na bidii kubwa.




## QUR'AN TUKUFU


وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ اَزْوَاجًا وَّذُرِّيَّةً ؕ وَمَا كَانَ لِرَسُوْلٍ اَنْ يَّاْتِيَ بِاٰيَةٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ لِكُلِّ اَجَلٍ كِتَابٌ ﴿۳۹﴾

Na bila shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako, na Tukawapa wake na watoto. Na haiyumkini Mtume kuleta Ishara isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unayo hukumu iliyoandikwa. 13_SURA_AR-RA'D_: 39



## NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na hazrat Abdullah bin Amri r.a. ya kwamba, mjumbe wa Allah s.a.w.alisema: Atashuka Isa bin Mariam kwenye ardhi, basi ataoa na atajaliwa kizazi(cha kutumukia dini) na atakaa ardhini miaka arobaini na mitano (yaani baada ya kutangaza madai ya kwamba ametumwa). Kisha atafariki na atazikwa Pamoja nami katika kaburi langu. Hivyo mimi na Isa bin Mariam tutainuka kutoka kaburi moja baina ya Abu Bakr na Omar.



## Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Sheikh Akbar (Hadhrat Muhy ud din Ibn Arabi RH.A.) alisema: Isa a.s. atashuka baina yetu akiwa hana sheria lakini atakuwa Nabii bila shaka.

( Futuhate Makkiyah:J.1.uk:57)

Masih e Maud A.S. Anasema: Mjumbe wa Allah[saw].alitoa bishara kuwa: Masih Aliyeahidiwa atoa kwa yakini na kujaliwa kizazi. Kwa hakika kuna dokezo ndani ya maneno hayo kwamba: bila shaka Mwenyezi Mungu atamjalia Mtoto mwema atakayefanana na baba yake, wala hatakuwa kinyume chake na atakuwa miongoni mwa watu wenyeheshima sana kwa Mungu.

( Aaina e Kamalate Islam, R.Kh.J.5.uk:578)

Kisha Misihe Maud[as]. anasema: kuna ishara ndani ya bishara hii kwamba, Masih aliyeahidiwa atapata mwana mwema atakayefanana naye katika ubora na fadhila zake.(TuhfaeBaghdad, R.Kh.J.7.UK:209)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

# AHADI YA KIHISTORIA YA MWANA ALIYEAHIDIWA

## Na jinsi alivyotekeleza ahadi ile

**Na.**
**Sh. Abdul Nasir Bajwah**
**Jamia Ahmadiyya Tanzania**

**مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللهَ عَلَيْهِ ۖ فَمِنْهُم مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ ۖ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا**

**(الاحزاب:24)**

Wapo watu miongoni mwa waaminio waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu: hivi baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea, wala hawakubadilika hata kidogo. (33:24)

Kwa kuomba msaada kwa Allah nitajaribu kubainisha kuhusu "Ahadi ya Mwana Aliyeahidiwa رضی اللہ عنہ (Mwenyezi Mungu Awe radhi naye)، kwa Allah سبحانہ و تعالیٰ wakati wa kifo cha Masihi Aliyeahidiwa علیہ السلام na jinsi alivyotekeleza ile ahadi maisha yake yote."

Kila mwaka Tarehe 20 mwezi wa pili sisi tunasherehekea Siku ya Mwana Aliyeahidiwa na vile vile wenzetu wanajumuiya wote duniani kote mahala popote wanaendelea kuadhimisha siku hii kwa heshima na taadhima zote.

Kwa nini tunasherehekea siku hii yaani siku ya Mwana Aliyeahidiwa? Kwa nini hatuadhimishi siku zinazohusika na makhalifa wengine?

Katika kujibu swali hili Khalifa wetu mtukufu أيده اللہ تعالیٰ بنصرہ العزیز anasema:

"Siku ya Bishara ya Mwana Aliyeahidiwa tunaadhimisha ili tuweze kusisimua Imani yetu na tuweze kukumbushana ile ahadi ya kwamba lengo letu haswa ni kuimarisha ukweli wa Islam na Mtume Mtukufu صلی اللہ علیہ وسلم katika ulimwengu mzima. Siku hii sio siku ya kuzaliwa kwake au ya kufariki kwake. Bali katika siku hii kwa kukubali dua za Masihi Aliyeahidiwa علیہ السلام Mwenyezi Mungu Alionyesha ishara ya kwamba kutoka kizazi chake atazaliwa mtu mmoja mwenye sifa maalum na ambaye ataimarisha ukweli wa Islam katika dunia nzima, na kwa kupitia yeye njia mbali mbali zitapangwa kwa ajili ya Nidhamu ya Jamaat, njia ambazo kwa kuzitumia watu watakaokuja baadae wataendelea kupata maendeleo.

Basi daima siku hii inatukumbusha kutumia nguvu zetu zote kwa ajili ya maendeleo ya Islam pamoja na kutambua majukumu yetu, na ndivyo ilivyotakiwa iwe. Sio hii tu ya kwamba tupate hadhi ya kielimu tu kwa kutambua kutimia kwa ishara hii. Mwenyezi Mungu Atujaalie uwezo."

*(Hotuba iliyotolewa Tarehe 20 Feb 2009, iliyochapishwa katika Alfazl 13 Mar 2009)*

***"Hata kama watu watakuacha na nibakie peke yangu, nitasimama nawe na nitakabiliana na upinzani wote na mashambulizi dhidi ya ujumbe wako. "***

Haya ni maneno yaliyotamkwa na Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad wakati wa kifo cha baba yake mpendwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s.

Wakati wa kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s., mtoto wake huyu alikuwa na miaka 19 tu, lakini maneno yake haya yalijawa na imani na uaminifu wa daraja la hali ya juu. Aliishi kwa miaka mingine 57 na katika umri wake wote huo kila maamuzi yake na tendo lake yalifanywa kwa kuzingatia kauli hiyo. Na kwa hiyo akatimiza ahadi aliyoitoa mbele ya baba yake na pia kwa kufanya hivyo ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s., kwamba atampatia mtoto atakayekuwa Musleh Mau'ud, ikatimia kwa shani na ukuu wenye kutukuka.

Baada ya kuzikwa kwa Masihi Aliyeahidiwa [as], Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad r.a alirejea nyumbani kwa uvumilivu mkubwa, nyumba ambayo ilikuwa imekosa baba yake mpendwa na Imam mtukufu wa zama, ambamo hapakuwa na hazina za kidunia wala hakumrithisha utawala wa kidini wa aina yoyote. Yaani nyumba tupu.

Hata hivyo, mama yake mheshimiwa Hazrat Nusrat Jahan Begum r.a aliwaambia watoto wake kwamba kwa kweli nyumba hii haikuwa tupu. Hadhrat Amma Jan [ra] (Mama yake Hadhrat Sahibzada Sahib) amesema:

"Enyi Watoto! Msifikirie kwa kuangalia nyumba tupu, kuwa baba yenu ameondoka bila kuwaachia cho chote. Ameacha kwa ajili yenu hazina kubwa za maombi Mbinguni ambazo zitaendelea kupatikana pamoja na fadhila za Mwenyezi Mungu na baraka zake katika maisha yenu yajayo."

Kwa hivyo, hadi leo tunashuhudia kuwa kizazi cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. kinaendelea kupata hazina zile za kimbingu katika sura ya neema ya Mungu.

Hazrat Musleh Mau'ud (ra) Katika kuzungumza kuhusu ahadi ile alisema;

"Ilikuwa ni wakati wa mwisho mwisho katika maisha ya Masihi Aliyeahidiwa kabla ya kifo chake, na wanaume wengi walikuwa wamekusanyika karibu na kitanda chake, wanawake walikuwa wameshaondoka hapo. Watu pande zote tatu walikuwa wamezunguka kitanda chake. Nilitengeneza nafasi na kusimama upande wa kichwa …

"Niliona kuwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alifungua macho yake, alitazama hapa na pale na kuzifunga. Tena akafumbua macho yake na alijitahidi kuangalia

# AHADI YA KIHISTORIA YA MWANA ALIYEAHIDIWA

## Na jinsi alivyotekeleza ahadi ile

pande zote... Alirudia hili mara nyingi. Mwishowe alikusanya
nguvu zake zote kwa mara ya mwisho kwa sababu mtu anapokaribia kufariki anakuwa mdhaifu sana, alitazama tena pande zote, wakati macho yake yalipoona mimi….., ilionekana kana kwamba alikuwa ananitafuta mimi. Na alijisikia faraja kwa kuniona mimi. Baada ya hapo akafumba macho, na akafariki. Wakati huo nilihisi ya kwamba macho yake yalikuwa yananitafuta mimi tu. Na mimi nilifikiria kuwa haya yalikuwa matokeo ya maombi yangu mimi kutazama macho hayo kwa mara ya mwisho.

"Mara baada ya kifo chake baadhi ya watu walikuwa na wasiwasi kuhusu siku za mbele ya kwamba sasa kitatokea nini... itakuwaje kwa Jumuiya?

Ingawa nilikuwa na umri wa miaka kumi na tisa tu wakati huo, nakumbuka nilikuwa ninasimama karibu na maiti takatifu ya Masihi Aliyeahidiwa na nilisema:

'Ee Mola wangu, mimi kwa kuamini kuwa wewe ni Mjuzi wa kila kitu, naahidi kwamba hata kama wanajumuiya wote wataiacha Ahmadiyyat, mimi nitafikisha katika kila kona ya dunia ujumbe ule ambao umeudhihirisha kwa kupitia nafsi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s."

Huzur r.a anasema; "Mtu hupitia hali tofauti tofauti katika maisha yake. Kuna hali ya uvivu, ya umakini, ya maarifa, ya ujinga, ya utii kwa Mungu na ya uzembe pia. Lakini hadi leo nahisi hiyo kwamba ile hali ilikuwa ya umakini wa daraja la juu na ya maarifa ya kina ya Mwenyezi Mungu kwamba kila kipande cha mwili wangu kilishiriki katika ahadi hiyo.

Nilikuwa na uhakika ya kwamba nguvu na heshima zote za ulimwengu wote hazikuwa na umuhimu wo wote mbele ya dhamira, azimio na ahadi yangu ile.

Ikiwa ulimwengu ungeweza kusikia hisia na dhamira yangu bila shaka wangelichukulia kuwa kauli ya mtu ambaye amepoteza akili yake. Hata hivyo, Nilikuwa na imani ya kwamba ahadi yangu hii ni jukumu langu kuu. Na wakati nilipofanya ile ahadi nilikuwa najua moyoni mwangu ya kwamba ahadi hii haikuwa nje na uwezo na nguvu nilzozijaliwa na Mwenyezi Mungu."

*(Fazl-e-Umar by Mujeeb-ur-Rehman, Page. 98-100)*

Hazrat Nawab Mubaraka Begum r.a. binti wa Masihi Alyeahidiwa a.s. sehemu moja alisema;

Ahadi ambayo aliifanya mbele ya maiti ya Masihi Alyeahidiwa a.s, aliitekeleza kama ilivyotakiwa. Na msaada wa Mungu ulikuwa unaonekana katika kila hatua; Kazi zake za kuandika maelezo ya Qur'an, darasa zake za Qur'an, maandishi na kauli zake, hotuba zake ni hazina kubwa na yenye thamani. Zaidi na hayo uwezo wake wa kufanya kazi yo yote, uwezo wake wa *ajabu ya* kutoa maamuzi *kuhusu mambo mbali mbali*, nia madhubuti, kuiongoza jumuiya katika kila hatua, kujenga vituo vya Islam Ahmadiyyat katika kona zote za dunia, ilhali katika kila jambo lake tunashuhudiayakwamba Mwenyezi Mungu alimjaalia Roho maalum na ya ajabu. Fadhila za Allah na Rehema zake ziliendelea kubaki naye. Hata adui yake hawezi kukataa kazi zake kubwa alizozifanya yeye. Kijana mwenye afya dhaifu, ambaye alimdhihirisha Mwenyezi Mungu, aliwashinda wasomi na viongozi wengi wa daraja la juu. *Hazrat Khalifa-tul-Masih wa pili r.a.* aliweza kuzifanya kazi zile za ajabu ambazo Waislamu wote kwa ujumla pamoja na mali zao na elimu yao yote wameshindwa kuzifanya…

*(Tarikh-e-Ahmadiyya J4, U3)*

Kama tunaangalia athari za Kiroho na ya Kidini ya zama za Ukhalifa tunagundua kuwa ni ya kimataifa. Hazrat Musleh Mau'ud r.a. mwenyewe alisema;

"Mimi ni Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s, kwa hiyo mimi ni khalifa kwa ajili ya watu wa Afghanistan, bara la Arabu, China, Japan, Ulaya, Marekani, Afrika, Samtra, Java, na Uingereza pia, yaani mimi ni Khalifa kwa ajili ya Ulimwengu mzima. Katika jambo hili watu wa Uingereza pia ni chini ya utawala wangu na hakuna nchi yo yote wa dunia ambayo sio chini ya utawala wangu wa kidini, kwa hiyo hii ni amri kwa wote kuwa wafanye baiati yangu na waingie katika Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

*(Tarikh-e-Ahmadiyya J4)*

Basi maendeleo ya Islam ya zama hii na yajayo yatapatikana pamoja na Ukhalifa huu wa kitaifa na utawala huu wa kidini tu. Kama alivyosema;

"Basi muda huu Mweneyzi Mungu amelazimika maendeleo ya Kiislam pamoja nami, kama daima anaambatanisha maendeleo ya kidini pamoja na makhalifa wake. Basi yule ambaye atanisikia atafaulu, na ambaye hatanisikia atafeli. yule ambaye atanifuata, Mwenyezi Mungu Atamfungulia milango ya Rehema na ambaye atajitenga na mimi, atakosa Rehema ya Mungu.

*(Tarikh-e-Ahmadiyya J4)*

Nabii[saw] kwa idhini na msaada wa Allah[sw] kwa kupitia mafundisho yake anapanda mbegu. Na makhalifa wake baada yake wanalinda ile mbegu na wanatengeneza mazingira yanayo inasaidia ile mbegu kubadilika katika mti madhubuti.

Naamini wengi wetu kwa namna moja au nyingine tunatambua

# AHADI YA KIHISTORIA YA MWANA ALIYEAHIDIWA

## Na jinsi alivyotekeleza ahadi ile

kazi ya kulima, mkulima kabla ya kupanda mbegu anaandaa ardhi. Kama ardhi inakuwa ngumu anapalilia, anakatua katua, anasawazisha, tena kama ardhi inakosa nguvu anachanganya mbolea, kisha anapanda mbegu. Wakati mbegu imeshapandwa, muda ule ni muda wa kuwa makini zaidi. Hali ile inakuwa dhaifu mno.

Vile vile baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. hali ya jumuiya ilikuwa. Fitna ya wale waliokuwa wanapinga Ukhalifa, uchochozi wa wapinzani na pia uchache wa idadi ya waaminio, mambo haya yote alikabiliana kwa ujasiri mkubwa. Upande moja aliimarisha Ukhalifa kwa kumfuata Khalifa mtukufu wa 1 r.a, kwa kumtii, kwa kumsaidia kwa namna moja au nyingine katika kulinda ule mbegu uliopandwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na upande mwingine alitengeneza mazingira yanayofaa kwa ajili ya mbegu ule kukuwa katika sura ya mti madhubuti. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu aliweka misingi ya nidhamu ya ajabu ambayo inaunganisha wanajumuiya katika mnyororo moja madhubuti.

Nidhamu hii inafanana na nidhamu ya damu katika mwili wa binadamu. Upendo kwa khalifa, upendo kwa mitume ya Allah, upendo kwa dini na upendo kwa Allah, hizi zote zinatembea kama damu katika jumuiya nzima kwa kupitia Nidham ya Jamaat.

**Waaminio wenzangu!**

Leo sisi ni mashahidi wa jambo hili ya kuwa nani alikuwa anafuata haki, wale ambao walikataa Ukhalifa au wale ambao walifanya baiati siku ile. Msaada wa Allah unadhihirisha ukweli wazi wazi. Leo tukiwa hapa katika nchi ya Afrika Mashariki tunaendelea kumkumbuka yule mwana wa ahadi ambaye mwenyewe alisema

**اک وقت آئے گا کہ کہیں گے تمام لوگ**
**ملت کے اس فدائی پہ رحمت خدا کرے**

Utafika wakati ambapo watu watasema, Mwenyezi Mungu Amrehemu mpenzi huyu wa Ummati huu.

**اللھم ارحمہ برحمتک الواسعۃ،**
**اللھم ارحمہ برحمتک الواسعۃ،**
**اللھم ارحمہ برحمتک الواسعۃ۔**

Leo dunia nzima watu wanaendelea kutoa ushahidi ya kuwa Huyu huyu Mwana wa ahadi ni Musleh Mau'ud sawa na utabiri ule uliotolewa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na upande mwingine leo hakuna mtu ambaye anawajua wale ambao walikataa Ukhalifa. Na hii pia ni hisani ya Mwana Aliyeahidiwa kwao kuwa sisi waahmadiyya pekee ndiyo wanaowataja majina yao leo.

Kwa Neema ya Mwenyezi Mungu zama za Ukhalifa wa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad [ra] iliendelea zaidi ya nusu karne na ilijaa na matukio mengi ambayo yalihusu nyanja mbali mbali za mtu binafsi, za jumuiya, maisha ya kitaifa na kimataifa. Kubainisha historia yote ya zama za Ukhalifa wa pili inahitaji muda usiohisabika. Kwa hiyo nitajaribu kugusa baadhi ya mambo kwa kifupi yatakayoeleza utekelezaji wake wa ahadi ile aliyoifanya na Mwenyezi Mungu katika sura ya kutumikia haswa Islam Ahmadiyyat na kwa ujumla Ubinadamu.

Kwa mfano alianzisha, Gazeti la Al-Fazl, Tehrik-e-Jadid, Waqf-e-Jadid, Nidhamu ya Tandhim zote, Answarullah, Khuddam-ul-Ahmadiyya, Atfal-ul-Ahmadiyya, Nasira-tul-Ahmadiyya, Lajna Imaa'illah, Majlis Shura, Darul Iftaa; yaani chombo cha kupata fatwa kuhusu mambo mbali mbali yanayohusika dini, Darul Qadhaa; chombo cha kusuluhisha migogoro mbali mbali n.k. Ujenzi wa Mnara wa Masihi pia ulikamilika katika zama zake.

Katika kutekeleza ahadi ile alijitahidi sana, katika zama zake Jumuiya ilienea katika nchi takriban 70 na. Wabashiri waliandaliwa kisha walipelekwa katika nchi nyingi za bara zote.

Sasa nitajaribu kuweka mbele yenu muhtasari wa kazi zilizochapishwa za Mwana Aliyeahidiwa[ra].

Khalifa Mtukufu[atba] katika hotuba yake ya Ijumaa Tarehe 17 mwezi wa pili 2023 akielezea kazi zake alisema; kwamba vitabu vyake, hotuba, mihadhara ya Mwana Aliyeahidiwa r.a, ambayo yamechapishwa katika mfumo wa kitabu au yako tayari kuchapishwa idadi zao ni 1,424. Zinapatikana katika muundo wa seti iitwayo Anwarul Uloom ambayo ina juzuu 38. Jumla ya kurasa ni 20,340. Khalifa Mtukufu (aba) alisema; tukihisabu Tafsir-e-Kabir (Maelezo makubwa) na Tafsir-e-Saghir (Maelezo madogo) pamoja, jumla ya ukurasa zinazojumuisha kazi zake za Maelezo ya Qur'ani Tukufu inafika ukurasa 28,735. Alitoa 1,808 Hotuba ya Ijumaa, ambayo ina kurasa 18,700. Alitoa Hotuba 51 za Eid al-Fitr ambazo zina kurasa 503. Alitoa Hotuba 42 za Eid al-Adha zenye kurasa 405. Alitoa hotuba 150 za Nikah, (yaani tangazo la ndoa) ambazo zina kurasa 184. Hotuba yake katika Mkutano wa Shura pia zimechapishwa ambazo zina kurasa 2,131. Kuna aina nyingine pia ya maandishi yake zinapatikana, tukihisabu ukurasa zote za kazi zake, zinafikia kurasa 75,000.

**سبحان اللہ وبحمدہ سبحان اللہ العظیم**

Khalifa Mtukufu (aba) alisema; imedhihirika kuwa Hazrat Musleh Mau'ud (ra) alikuwa na baadhi ya machapisho katika Al-Fazal na Al-Hakam ambayo bado hayajajumuishwa katika Anwarul Uloom. Kuna makala 55, hotuba 27, vipindi 43 vya maswali na majibu, kaulli zake 220 zilizorekodiwa, na barua 131 imepatikana

# Bustani ya Washairi

Kilio cha Wasitafu
Bisimilahi naanza, kwa jina la wetu Mumba
Kaumba mbingu ya kwanza, bila hata ya miamba
Na aridhi katandaza, viumbewe kujigamba
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Muda mrefu sasa, tukipatacho ni haba
Tumaini hasahasa, nyongeza iso haba
Ikonge mioyo hasa, na kuondoa magamba
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Sikia Wasitafu, ni mengi waliyakumba
Walikuwa wadilifu, walipambana si haba
Kwa nchi yao wanyofu, bila hofu wakajenga
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Mama yetu mtukuka, mlezi wetu wa wana
Mkuu wa nchi husika, mwemye wema ya bayana
Salamu zitakhfikia, za wako wapendwa wana
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Mama yoo twatamka, kilio cha wako wana
Ni maji yametufika, shingoni yamebanana
Twamuombea msifika, Mola ampe baraka.
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Sita beti zimefika, nimeziweka bayana
Raisi ni msifika, ni mwema alobayana
Hana kinyongo hakika, twamuomba aendelee
Kilio cha Wasitafu, hali duni ya kipato.

Harun R. Bundara (Msitaafu)
Kiloleni, S.L.P 54 Tabora
0783257566

## IPE ZAWADI DUNIA

Naipa zawadi dunia, Mimi kuwa mja mwema
Kheri naimiminia, Siku kucha kujituma
Salama naifikishia, kuhini wangu mtima
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Kwa dhamira najipinda, Kumpata Muumbaji
Maumivu nayasunda, Kutimiza langu hitaji
Naubeba Mzigo punda, Ukifika uponyaji
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Nakanyaga mule mule, Kwenye chapa zenye damu
Walipokanyaga wateule, Tangu enzi za Adamu
Nami wao msukule, Kuitafuta hatamu
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Jama mie nadurusi, Kurasa za micharazo
Naweka nyuma fulusi, Ya amri na katazo
Nasoma najinafasi, Kwenye hekima na vigezo
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Uvivu ni yangu theluthi, Kwa juhudi naukwepa
Nataka kuacha urithi, Kwa kumbukumbu kuwapa
Hivyo ziwezi hanithi, Malengo niliyojipa
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Mie nyuma ya walitotangulia, Sinacho kiherehere
Wana mengi wamepitia, Haifai tuwakere
Heko wametumikia, Najishusha mie ngedere
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Mie sikio liwazi, Nasikiliza waadhi
Si mwingi wa maongezi, Wala wa nzuri lafudhi
Ukishauri siongezi, Kwa amali nahifadhi
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Kamwe siwezi kuumwa, Shimo moja mara mbili
Mara moja nikisemwa, Huwa nachaji akili
Mapema huwa nahemwa, Nikiharibu amali
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Kwenye mipango mpole, Nina subira na shauku
Mwili hunioti upele, Kwa porojo za kasuku
Kama havisongi mbele, Narusha Mishale usiku
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Ukimtaka mzuri, Jijenge wewe mmoja
Jizinge rohoni nuri, Majaribu uwe soja
Mhanga uwe tayari, Dunia inakungoja
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

Dua jambo muhimu, Huliumba kila jambo
Omba usiishwe hamu, Jivike utoto kambo
Jitoe akili timamu, Huduma jitoe chambo
Dunia yataka afua, Kwa kuwa na waja wema

**Shunda mshundia wana**
**Daluni-Tanga**

# BENDERA 19 ZA SHUSHWA YAPANDISHWA YA AHMADIYYA.

**Na. Mwana Historia wetu**

Maskini binadamu. Kiumbe mzito hachukuliwi na wala habebeki. Ni dhaifu kweli kweli. Ukumbusho haumsaidii. Jana haifanani na leo yake. Vitabu vitakatifu vimeleeza mwisho na maangamio walioyapata waliokadhibisha. Lakini wapi, la kuvunda halina ubani, Wameweka pamba masikioni na kujifunza hawawezi. hata uchukue takilifu ya kumfungulia Saifu za vitabu ni kazi bure kwake. Ni jani lililodondoka kutoka kwenye mti. Hatima yake ni kuoza na kuwa Mbolea.

Nani angefikiri kwamba baada ya zilzalaha iliyowapata watu wa Lindi walioambiwa kuwa Allah atashuka na akashuka kweli katika sura ya kimbunga. Watu baada ya kusikia na kuelezwa yaliyokumba mji wasingediriki tena kuchezea askari wa mtukufu Mtume Muhammad[saw] ambao wanaongozwa na Amiri jeshi masih aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad. Lakini wapi sikio la kufa halisikii dawa. Mwezi wa tisa mwaka 1977 jumuiya ya Ahmadiyya ilitangaza kuwa itafanya mkutano wake wa mwaka katika mji wa mtama.Habari hizi zilipokelewa kwa ghadhabu na hasira na maulamaa wa sehemu hii ya Tanzania. Kweli walikuwa wanaisikia Ahmadiyya kweli walikwisha ona vitubu vyao ,hi ni Dhahiri walishasikia simulizi juu ya mtama. Sheikh Fadhilillah Bashir ambaye alipewa Simba na Allah ili imsindikize. Yote hayo walikuwanayo moyoni kwa uchungu mkubwa lakini sasa hawa walikuwa wamefurutu ada.Tumewakaribisha sebuleni sasa wanataka kuingia chumbani. Hatukubali hatukubali ng'o.

Mipango ikafanywa ya kutafuta bendera.Bendera tisa zikapatikana na watu wakapita mitaani kwajazba kubwa wakilaani na kueleza kwamba wataendesha dua ya kuwasambaratisha na kuwamaliza waahmadiyya. Hakufanikiwa Zia ul Haq aliyekuwa na majeshi senze na hawa waliokuwa hawana hata gobole. Kwa mzee maarufu wa mjini mtama walioweka kambi wakizikiri kuomba dua na kulaani waahmadiyya. Dua la kuku mwewe huyo anabeba kifaranga hewani. Mkutano ulifanyika tena kwa mafanikio makubwa.Hilo lilikuwa pigo la kwanza kwa maadui wa Mtume[saw] ,la pili lilikuwa zito zaidi na ishara pale walipoweka kambi pale walipofanya kituo cha kurushia makombora dhidi ya Ahmadiyya Allah atafanya sehemu hiyo kuwa mali yetu.

Miezi mitatu baada ya tukio hilo lenye mbwembwe nyingi mwenye nyumba anafariki.makubaliano yalifanyika miongoni mwa Watoto wa marehemu. Na tizama Allah alivyo ***Shadidil ikab***-mkali wa kuadhibu. Nyumba hiyo alinunua mwanajamati Saidi Kalindima na kuipatia jamati.sasa pamejengwa msikiti na mara tano inatoka adhana inayonadi umoja wa Allah na ukweli wa mtukufu mtume Muhammad[saw].

# P E P O D U N I A N I

*Kutoka toleo lililopita*



*Maulana Sheikh Shaban A. Shunda*

**UchaMungu na ana uhusiano mzuri na Mungu, ana furaha ya milele inayotokana na kuwa na imani".**

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (5)**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa[as] alisema kuwa: "Mambo yote ya ulimwengu huu yanakabiliwa na mabadiliko na mageuzi. Dhiki mbalimbali huja kwa mtu. Magonjwa hushambulia. Wakati mwingine watoto wa mtu hufa. Kwa kifupi, shida fulani au nyingine, maumivu, huzuni fulani. Dunia hii ni mahali pa shida na mambo haya humnyima mtu usingizi kwa urahisi. Kadiri duara la mahusiano ya mtu linavyoongezeka, ndivyo wigo wa shida na dhiki unavyoongezeka. Kadiri mduara wa uhusiano unavyoongezeka kupitia hatua tofauti, shida hizi zinaweza kutengeneza huzuni hamsini zaidi kutoka huzuni moja. Ikiwa mtu yuko peke yake, atakuwa na wasiwasi mdogo lakini akiwa na mke, watoto, wazazi, dada, kaka na mahusiano mengine, basi shida ndogo inakuwa shida kwake. Kwa kuzingatia jumla ya mahusiano haya, mtu angeweza kupata furaha tu ikiwa hakuna mtu (kutoka kwa mzunguko wake wa mahusiano) aliyeugua au alipata dhiki au shida yoyote".

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (6)**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) alisema kuwa; "**Wazo kwamba utajiri huleta furaha pia sio sahihi**. Furaha haiji kwa mali pekee yake. Ikiwa afya ya mtu si nzuri au, kwa mfano, mtu anaugua tumbo vibaya, je, hayo yatakuwa maisha ya pepo? Kwa hiyo, tunajifunza kutokana na hili kwamba utajiri sio chanzo cha furaha. Ukweli ni kwamba mtu ambaye ana uhusiano na Mungu, ndiye ambaye, kwa kila jambo, anafurahia maisha katika pepo (maisha ya furaha ya kweli). Hii ni kwa sababu Mungu ni muweza wa yote na ana uwezo wa kumweka mbali mtu na kila aina ya magumu na pia uwezo wa kumlinda dhidi ya mateso yanayosababishwa na matatizo ya kifedha. Matatizo kama hayo yakitokea, basi Mungu hutupatia uwezo wa kuyakabili kwa ujasiri na nguvu.

Jumla ya vipimo ambavyo ni muhimu kwa ustawi wa mtu havimilikiwi (na mtu yeyote), hata mfalme. Haya yote yako mikononi mwa Mmoja tu, Mfalme wa Wafalme, ambaye humruzuku amtakaye. Wakati fulani inazingatiwa kuwa kuna aina ya watu ambao wana mali nyingi lakini wanakuwa wahanga wa magonjwa kama vile ulaji (arosto ya kupenda kula), na maisha yao yanakuwa machungu sana. Kwa hivyo, ni nani anayeweza kushughulikia mamilioni ya shida ambazo anazo mwanadamu? Ikiwa kuna huzuni, ni nani awezaye kumpa mtu uvumilivu? Ni Mungu peke yake anayeweza kufanya hivyo".

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (7)**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) alisema kwamba: "Uvumilivu ni jambo kubwa ambalo haliruhusu huzuni kubwa kuja karibu hata wakati wa shida na dhiki kubwa. Kuna baadhi ya matajiri ambao katika kipindi cha raha na starehe wanakuwa na kiburi sana na kujawa na umuhimu wa kibinafsi lakini kwa kufikwa shida kidogo hulia kwa sauti kama watoto. Hatumjui mtu yeyote ambaye hajaathiriwa na ajali fulani na ambaye uwepo wake haujapata huzuni".

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (8)**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) aliseme: "Maisha ya nani ni pepo? Ni ya mtu yule tu ambaye ana baraka za Mwenyezi Mungu. Ndio maana ni kosa kubwa sana kuona mtu amevaa nguo nyeupe, watu wanasema mtu kama huyo ni wa mbinguni (peponi). Ikiwa ungewauliza watu kama hao watakuambia juu ya dhiki nyingi ambazo wamelazimika kukabiliana nazo. Kuchunguza tu nguo za mtu, au kuwaona wakiendesha gari au kunywa pombe na kudhani (kwamba wana furaha na wanaishi peponi) sio sahihi. Zaidi ya hayo, maisha ya uhuru kamili, yenyewe ni maisha ya kuzimu. Je, inaweza kuwa zaidi ya maisha ya kuzimu kuliko maisha ambayo hakuna heshima kwa Mungu na hakuna uhusiano na Mungu. Mbwa anaweza kula kitu kilichokufa au anaweza kutenda vibaya (yuko huru kufanya hivyo) — Je, haya yatakuwa maisha ya peponi? Kadhalika, mtu anayekula maiti na akafanya vitendo vya kifedhuli, ambaye hajui kutofautisha mali ambayo ni halali, (yaani iliyopatikana kwa uhalali) na ambayo ni haramu (yaani iliyopatikana kwa haramu), haya yatakuwa ni maisha ya laana ambayo hayana mfanano wowote na maisha ya peponi".

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (9)**

Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) aliseme: Ni kweli kwamba maisha ya peponi ni mamoja (ambamo mtu anakingwa dhidi ya maovu yote) lakini ni kwa wale tu wanaomtegemea Mwenyezi Mungu kikamilifu na hivyo kwa mujibu wa ahadi aliyoiweka Mwenyezi Mungu katika aya isemayo 'Na Yeye (Allah). huwatunza wenye UchaMungu', **(Q.7:v.197)**, yaani, wanakuwa chini ya ulinzi na utunzaji wa Mungu. Kwa upande mwingine, siku za mtu aliyetenganishwa na Mungu hupitishwa kwa hofu na mawazo ya matamanio. Hawezi kuwa na furaha. Kulikuwa na mtu huko Sialkot ambaye alikuwa akipokea hongo. Alikuwa akisema kwamba alichokuwa akiona ni pingu tu (mikononi mwake). Ukweli ni kwamba tendo baya linapaswa kuwa na mwisho mbaya. Ni kwa sababu hii kwamba nafsi haiwezi kamwe kuridhika na matendo mabaya. Basi, iko wapi raha ya matendo maovu? Tukio la kila tendo baya linabana moyo na mtu anahisi uzito juu yake na analazimika kujiuliza, 'Ni upumbavu gani huu?' Na matokeo yake anajilaani. Pia wanafikia viwango vya kutisha, mtu mmoja aliua mtoto kwa ajili ya sarafu chache (kwa sababu ya msongo wa mawazo)!"

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

**PEPO DUNIANI (10)**

Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: "Kwa kifupi maisha si chochote ila ni kujilinda na matendo mabaya na kumtegemea Mungu kwani anayemtegemea Mungu kabla matatizo hayajamkabili, yeye ndiye husaidiwa na Mungu wakati wa shida. Anayelala kabla ya taabu kumpata, huangamizwa wakati wa taabu. Mungu hahitaji chochote kutoka kwa mtu yeyote. Maeneo kama vile Bicaneer yalipokumbwa na ukame, watu huko walifikia hatua ya kula watoto. Hii ilitokea kwa sababu hawakuishi maisha yao kwa kujikabidhi kwa mungu. Kama wangeishi kwa ajili ya Mungu, watoto hawangepatwa na hali hii. Ni wazi kutokana na Hadith (hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (sa) na kutoka katika Qur'ani Tukufu na vilevile kutoka katika Vitabu Vitakatifu vilivyotangulia kwamba matendo mabaya ya wazazi wakati fulani huleta balaa kwa watoto. Aya ya Qur'ani Tukufu 'Hakujali madhara yake' **(Q.91:v.16)**, inaelekeza kwa hili kwamba wale wanaotumia maisha yao kwa uzembe, Mungu pia anakuwa mzembe juu yao. Unaona, mtumishi ambaye hamsalimu bwana wake kwa siku chache, humchukiza bwana wake. Kwa hivyo, kwa nini Mungu amjali yule anayevunja uhusiano wake Naye. (Ni kwa mtazamo huu kwamba) Mwenyezi Mungu anasema kuwa anawaangamiza na wala hajali vizazi vyao. Kutokana na hili inaweza kufahamika kwamba mtu MchaMungu anapokufa, akiwa amefanya wema katika maisha yake, Mwenyezi Mungu humjali hata kizazi chake kama inavyoonekana katika aya (ya Qur'ani Tukufu, inayosema kwamba) 'Baba yao alikuwa mtu Mcha Mungu' **(Q.18:v.83)**. Kwa ajili ya Uchaji na uwezo wa baba huyu, Mungu aliwafanya manabii wakubwa kama vile Musa (as) na Khizr wafanye kazi, kutengeneza ukuta ambao sasa ulikuwa wa wanawe. Ni hadhi kubwa kiasi gani mtu kama huyo anapaswa kuwa nayo (mbele ya Mungu)! Mungu alifunika hali halisi ya wana kwa kutotaja maelezo yoyote kuwahusu kwa sababu ingegeuza kutoka kwa sifa ya baba yao na pia kwa sababu Mungu alifunika (maelezo ya wana) kwa ajili ya baba yao. Mada hiyo hiyo imetajwa katika Vitabu Vitakatifu vilivyotangulia ambapo (Mwenyezi Mungu amesema) kwamba yeye huchunga hadi vizazi saba vya kizazi cha mtu mwema. Nabii Daud (as) pia amesema kuwa hajawahi kuona watoto wa mtu mwema wakiomba omba chakula. Kwa ufupi, furaha ya kweli ni riziki ('rizq') kutoka kwa mwenyezi Mungu ambayo haitolewi kwa wale wanaobaki nje ya pambo la utiifu kwa Mungu".

**(Malfoozat, Juz. 3, Uk 331-337 --16 Aug 1902).**

# Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam

*Na. Swaleh Kitabu Pazi*

***...Kutoka toleo lililopita***

ya kidunia. Ile hali ya wasomi kujihesabu kuwa ni watu fulani maalum katika jamii, ilikuja kuondoshwa na nidhamu adhimu ya jamaat Ahmadiyya. Tangu zama za Masihi Aliyeahidiwa imeshuhudiwa jinsi wasomi wakubwa wa fani nyingi za kidunia, walivyoepukana na kiburi na kuishi maisha ya unyenyekevu kwa kumthamini kila mtu. mfano mzuri wa watu wa aina hii ni pamoja na Maulvi Hakeem Nurud din, Sir Muhammad Zafrullah Khan, Mufti Muhammad Sadik[ra] na wengine wengi. Hawa walipata elimu kubwa za kidunia, lakini hawakujikweza kwazo bali walizitumia kwa ajili ya kujiongezea utambuzi juu ya Allah na kujipatia daraja za juu za kiroho.

Desturi hii imeendelea kurithiwa katika nidhamu ya jamaat, kizazi baada ya kizazi kupitia ukhalifa. Ili kuendeleza utamaduni huu wa watu kuiendea elimu kwa ajili ya manufaa ya Islam, jamaat imeanzisha tanzimu mbali mbali za ulezi wa makundi rika kwa ajili ya kuitumikia jamaat. Tanzim za jamaat, Majlis Ansarullah, Khudamul Ahmadiyya na Lajna Imaillah, hutumika kuwalea wanachama wake katika kila rika ili kuwaimarisha katika kuitumikia Islam, sawa na vipawa na elimu walizo nazo. Kama hiyo haitoshi, jamaat imeanzisha taasisi mbalimbali za kitaaluma ikiwemo ule umoja wa wahandisi na wasanifu wa majengo, IAAAE na nyinginezo. Ambazo huwakusanya wasomi wa fani mbalimbali na kuwashirikisha katika kuitumia elimu zao kwa ajili ya manufaa ya jamaat, Islam na jamii kwa ujumla.

Tofauti moja kubwa baina ya Jamaat Ahmadiyya na makundi mengine ya kiislam ni hii kwamba, katika jamaat kuna kiongozi mmoja mtukufu ambaye waumini wote humsikiliza na kumtii. Hivyo mtu hata awe na umaarufu, haiba na mamlaka makubwa katika jamii inayomzunguka, mbele ya nidhamu ya jamaat iliyo chini ya ukhalifa, hulazimika kuwa mnyenyekevu na mtiifu. Bila kujiali hadhi aliyo nayo katika dunia, msomi aliye chini ya ukhalifa huu hujitolea kwa uaminifu kutekeleza jukumu lolote apewalo na jamaat katika matukio mbalimbali bila kinyongo. Mfano mzuri wa hali hii huonekana wakati wa jalsa salana mbalimbali za kimikoa na kimataifa ambazo hufanyika kila mwaka kote duniani.

Aghalabu watu wasomi katika fani mbali mbali hupewa uongozi katika vitengo vyao vya kazi, na kwa hiyo vipato na heshima zao hutukuka kuanzia maofisini hadi mitaani mwao. Nje ya jamaat Ahmadiyya, watu hawa hupewa heshima maalum hata katika majumba ya ibada, na wakati fulani huhesabika kama wafadhili wa misikiti. Hii hutokana na baadhi yao kuwa na tabia ya kujitolea kifedha katika kadhia mbali mbali za kidini. Lakini hali ni tofauti katika jamaat yetu. Huku kila mtu hulazimika kujitolea kifedha sawa na kipato chake, hivyo kila mmoja wetu ni mfadhili wa jamaat. Awe msomi au asiye na elimu, awe tajiri au masikini na awe kiongozi au raia wa kawaida, wote huwa na wajibu ulio sawa katika suala la kujitolea kifedha. Hata wale wanaojaaliwa kuwa viongozi katika jamaat, hawachaguliwi kwa kuzingatia usomi wao wa elimu za kidunia, bali kiwango cha utawa na kujitolea kwao ndicho hufanywa kama kigezo katika uchaguzi wa viongozi wa jamaat. Jambo hili limeelezwa kwa upana mkubwa na msisitizo wa aina yake na Hazrat Khalifatul Masih V atba, katika hotuba yake ya ijumaa aliyoitoa Agosti 18, 2023, katika Masjid Mubarak huko Islamabad, Tilford – Uingereza.

Ujumbe mkuu uliobebwa na hotuba ile ulikuwa ni sawa na ile falsafa iliyohudhurishwa na maneno ya Mtume Mtukufu[saw]; sayyidul qaumi khaadimuhum (kiongozi wa uma ndiye muhudumu wao). Kun umuhimu mkubwa wa kila kiongozi wa jamaat, bali kila mwana jamaat kuisikiliza hotuba hii mara kwa mara. Hotuba hii inatoa somo adhimu siyo tu kwa viongoi wa jamaat pekee, bali kwa kila mwanajumuiya aliye kiongozi katika tasnia yoyote ya maisha. Ni lazima awe mfano wa uigwa kwa jamii anayoiongoza, aaepukane kabisa na kujikweza, maajivuno na kiburi kutokana na fanaka yoyote aipatayo kupitia elimu yake. Badala ya kuwa mtawala, anapaswa kuwa kiongozi katika utekelezaji wa kila jambo. Badala ya kujihisi yu mkuu, anapaswa kujishusha na kuonyesha upendo na unyenyekevu kwa wote walio chini yake.

Kila mwaka, tunazo kadhia kadhaa za kujifuza na kujizoeza desturi hii kupitiaa mikusanyiko ya jamaat. Katika vikao kama vile vya Jalsa Salana, Ijtimaa, Shura n.k, mifano ya kuigwa hupatikana juu ya tabia hii.

Tunayo mifano ya wasomi na watu maaarufu walivyojitolea kufanya kazi za chini mno, k.v. kuosha vyombo, kufanya ulinzi, kusafisha vyoo na mazingira katika jaalsa, bila kujali hadhi, elimu na nyadhifa walizo nazo.

Ni vyema ikieleweka kuwa namna njema ya kuiendea elimu sawa na mafundisho ya Islam, ni kutanguliza maslahi ya kiroho juu ya maslahi ya kidunia. Ni dhahiri kwamba watu wengi hutafuta elimu kwa ajili ya ama kupata ajira inayolipa zaidi, kupata heshima na madaraka makazini mwao, na wakati mwingine hujifunza taaluma za kibiashara kwa ajili ya kujiongezea kipato. Kwa ujumla ni kwamba utafutaji wa elimu kwa sasa huendewa kama biashara yenye tija kubwa inayoweza kumuokoa mtu na dhiki ya maisha ya dunia. Lakini Allah anatudokeza juu ya biashara inayopaswa kuendewa kwa jino na ukucha. Akiwaelekea waaminio, Allah Anasema kupitia Qur'ani Tukufu ya kwamba;

Yaa ayyuhal ladhiina aamanuu, hal adullukum 'alaa tijaaratin tunjiikum min 'adhaabin aliimun. Tu-minuuna billaahi wa rasuulihii wa tujaahiduuna fii

sabiilillaahi bi am-waalikum wa anfusikum; dhaalikum khairunl lakum in kuntum ta'lamuun.

Enyi mlioamnini! Je, niwajulisheni biashara itakayowaokoeni katika adhabu iumizwayo? Mwaminini Allah na Mtume wake, na mjitahidi katika nja ya Allah kwa mali zenu na nafsi zenu; hayo ni bora kwenu ikiwa mnajua. (61:11-12).

Hivyo kuiendea elimu kwa ajili ya kujijengea uwezo wa kujitolea sana katika njia ya Allah, linapaswa kuwa ndilo lengo kuu la kila mwanafunzi wa kiahmadiyya aliye katika ngazi yoyote ya elimu. Kwa njia hii, mafanikio yoyote ya kielimu yatakayofikiwa na mwana jumuiya, yatageuka kuwa kichocheo cha maendeleo yake ya kiroho. Kamwe hayatamsahaulisha wajibu wake wa kidini na kumfanya aigeukie dunia, kiasi cha kuihesabu kazi ya dini kuwa ni kazi ya wasiokuwa na jambo la maana la kufanya duniani. Haya ndiyo matumizi ya elimu yenye baraka kwa mujibu wa Islam. Lakini kuizamia dunia humfanya mtu aone kujitolea katika njia ya Allah ni kupoteza muda na nguvu bila faida yoyote. Mtu wa aina hii hutafuta mafanikio ya kidunia kwa nguvu, kasi na ari, akiamini kuwa ndilo lengo lenye faida kubwa. Lakini mwelekeo huu ndio wenye hasara mno kwa mujibu wa Qur'ani Tukufu, Allah Anasema;

Al ladhiina dhwalla sa'yuhum fil hayaatid duniyaa wa hum yahsabuuna annahum

yuhsinuunasw swun'a. uulaa-ikal ladhiina kafaruu bi aayaati rabbihim wa liqaa-ihii, fahabitwat a'maaluhum fa laa nuqiimu lahum yaumal qiyaamati wazna.

Ambao bidii yao imepotea katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanazifanya vyema sanaa. Hao ndio waliozikataa ishara za Mola wao na kukutana naye. Kwa hiyo vitendo vyao vimeharibika, wala hatutawasimamishia mizani siku ya kiyama. (18:105-106)

Ni maombi yangu ya unyenyekevu mbele ya Allah Atuwezeshe kuiendea elimu kwa lengo la kuisaidia jamaat yake ya kimbinguni. Na atuepushe kutumia elimu zetu kama ngazi ya kuyaendea mafanikio ya kimwili pekee, badala ya kuwa ngazi ya kupandia katika vidato vya madaraja ya taqwa.

Na neno letu la mwisho ni kwamba kila sifa njema zinamhusu Allah, Mola wa Ulimwengu.

# MATUKIO KATIKA PICHA

# VIJANA KUMI NA MOJA WAHITIMU MASOMO JAMIA AHMADIYYA-2023




Jamia Ahmadiyya ni moja ya idara muhimu sana iliyoasisiwa na Mtukufu Hazrat Masih-e-Mau'ud [as] kwa zaidi ya miaka 117 iliyopita. Hiki ni chuo kikubwa zaidi cha dini tukufu ya kiislamu kinachotoa elimu ya fani zote juu ya Islamu.

Tangu wakati huo hadi sasa, idara hii (Jamia Ahmadiyya)imefungua matawi yake katika nchi nyingi duniani ikiwemo pia Tanzania. Hapa nchini, mwaka wa masomo katika chuo hiki huanza katika mwezi wa Januari na kuishia mwezi wa Disemba kila mwaka kwa hafla maalum ya kuwaaga wanafunzi wanaomaliza masomo yao.

Mwa huu (2023) mahafali ya wahitimu yalifanyika mnamo siku ya Jumannne ya tarehe 5/12/2023 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 7:30 mchana katika ukumbi wa chuo uliopo kihonda mkoani Morogoro. Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni mheshimiwa Amir na mbashiri mkuu nchini-Maulana Sheikh tahir Chaudhry Sahib.

Hafla ilianza kwa usomaji wa Kurani Tukufu iliyosomwa na Mwalim Huessein Mpenda Omari na kufuatiwa na shairi la kiurdu lililosomwa na Nasrullah A. Amen na kisha kufuata na risala ya wahitimu iliyosomwa na Mwalim Juma Mwanyika. Katika risala yao wahitimu waliainisha changamoto kadhaa walizopitia na kutoa shukrani nyingi kwa mkuu (Principal ) wa chuo na safu yake ya viongozi kwa kuwalea na kuwaongoza vyema hadi kufikia hatua hiyo. Baada ya risala ya wahitimu, vijana waliofanya vizuri katika mashindano ya kielimu, walitoa hatuba katika lugha za kiarabu, kiurdu na kiingereza.

Baada ya hotuba hizo, ilifuata ripoti ya mwaka ya chuo katika lugha ya kiurdu, ambayo ilisomwa na Maulana Sheikh Azizi Ahmad Shahzad sahib. Ripoti hiyo ilionyesha mafanikio na maendeleo katika Nyanja za masomo, Tabligh, Waqar-e-Amar,michango,nk. Kisha ilifuata ripoti ya mwaka katika lugha ya Kiswahili.

Baada ya hapo, mgeni rasmi (Amir sahib ) alitoa zawadi kwa washindi wa fani mbalimbali kama vile katika mahubiri na uuzaji wa vitabu, michango, mitihani ya darasani nk.

Baada ya hapo, Amir sahib alitoa nasaha chache kwa wahitimu na wanafunzi wote kwa ujumla. Katika nasaha zake, Amir sahib alisisitiza sana juu ya suala zima la utii kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu 4:60 na kuwa wakweli katika kauli zao na vitendo vyao kama alivyoamrisha Allah katika Kurani Tukufu 33:71

Mwisho Amir Sahib aliwataka wahitimu kuzingatia na kujali hali na maendeleo ya wanajama'at katika mahubiri, michango, Tarbiyyat nk. Amesema kuwa huu ndio msingi wa majukumu ya kila mwalimu-popote awapo. Amir Sahib alimaliza hotuba yake kwa kuongoza maombi ya kimya na kufunga kikao.

Baada ya hapo sala za adhuhuri na Alasiri zilizaliwa kwa pamoja na mwisho washiriki walishiriki katika chakula cha pamoja.






# Jitafute Jitambue

*Na.*
*Maulana Sheikh Shaban A. Shunda*
*.....Kutoka toleo lililopita*



mkawa matajiri wote kwani ni jambo la muda tu, basi tungelikuwa mbali mno.

Wengine hufungua biashara au mradi na kuajiri ndugu zake ili kila mmoja apate kujiendesha huku wakielekea ndoto kubwa alizonazo mteule, cha kusikitisha waamua kufanya unyang'anyi na kumuua kabisa kiuchumi, na matukio ni mengi siku hizi yanayoonyesha ndungu wamemkatili ndugu yao kwa sababu hawapi hela wameamua kumuondoa duniani ili wazifaidi lakini badala yake umasikini umewarudia kwa ukali zaidi.

Kule kwetu daluni kwa sababu ni sehemu za machimbo ya madini basi watu huweza kuwa matajiri kwa haraka sana, kulitokea kijana mmoja alipata bahati hio, alikuwa na fedha nyingi, alioa mwanamke mmoja ambaye alikuwa ni fundi cherehani na kumfanya kuwa mwanamke mwenye hadhi kwa huduma nzuri alizompa, lakini badala yake dada Yule alihadaika na kuona zile huduma hazimtoshi akapewa mawazo na wapinzani wa mumewe katika biashara kuwa wamuue jamaa na yeye dada awe muendeshaji wa mali za kijana yule, dada aliafiki wazo hilo na kumuuza muwewe kwa wauaji, alipofanya hivyo tu baada ya muda alirudi kuwa fundi cherehani tena dhalili zaidi.

Jambo lingine mtu anapofuata wito wake hukutana na changamoto moja ambayo pia ni ngumu kwani huyayumbisha mawazo yake, na changamoto hiyo ni dharau, ikumbukwe kwamba watu wanaokujua vizuri ndio watu wa kwanza kutokukuamini, kwani wamekuzoea na wamekuona ukikua miongoni mwao, hata wazazi wetu huwa hawaamini kwamba tumekua na tunaweza kujiamulia jambo lolote lile, hivyo mara zote unapofanya maamuzi Fulani basi upinzani unaanzia kwa watu wa karibu wanaokujua, hivyo wengi wetu tunaathirika mno tunapoona maono yetu watu wetu hawayaoni. Kumbuka kwamba maono yako wewe ndio umepewa na Mungu, Mungu anaongea na wewe na sio wao, ile taswira ya unapoelekea hanayo yeyote miongoni mwao hivyo ukiwataka wayaone uyaonayo utajichelewesha.

Na jua kwamba kila mtu anafikiria anachokijua tayari, hivyo sio wote wanayo elimu inayowawezesha kufikiria kama wewe, uwezo wa ubongo ndio uwezo wa kufikiria na kila mtu yupo tofauti na mwingine hivyo hakuna kama wewe na usitake akuelewe yeyote kwani wengine huelewa kwa kuona kitu kimeshafanyika tayari.

Mteule anabidi asijitwishe wala asitwikwe mizigo mizito mpaka atakapofanikiwa kiwango cha kusaidia wengine, hili ni jambo muhimu mno katika kutafuta ndoto zako, pindi utakapoona hakuna msaada wa ndugu wala rafiki, kuitwa una roho mbaya sio kitu na wala sio kitu cha kuogopa, kila mtu Allah amemuwekea namna ya kupata riziki yake ikiwa mtu ni mzima wa afya basi ana uwezo wa kutatua changamoto za maisha yanayomzunguka, usijitwike mzigo mzito kwa kuogopa mashambulizi ya kihisia kutoka kwa ndugu na jamaa. Weka vipaumbele vyako na namna unaweza kumsaidia mtu huku ukijipa nguvu mwenyewe, kwani hata waliomtafuta Mungu walijitenga na watu wao na wakajitafutia utofauti, waliitwa kila namna ya majina mabaya lakini walijua wanachokihitaji: hadhrat Yusufu (as) alisema kuhusu maamuzi yake kwamba,

Hakika Mimi nimeacha mila ya watu wasiomwamini Mwenyezi Mungu, na wao hawaiamini Akhera. Na nimefuata mila ya baba zangu, Ibrahimu na Isihaka na Yakubu; hatuna haki ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na cho chote **(12:38-39)**

Historia ya Mtume (sa) ipo mbele yetu kwani alikuwa anaenda nje ya Mji na alikuwa hachanganyiki na watu ila kwa wale walio na silka na khulqa kama zake. Katika maisha ndugu au rafiki ni yule ambaye ataendana na ndoto zako ziwe za kiroho au za utafutaji wa kidunia wale wazito katika ndoto zako ni lazima uwape chaguo la pili.

Mtukufu Mtume (sa) anapoelezea athari za marafiki anasema:

"Mwanadamu anasukumwa na imani ya marafiki zake. Kwa hivyo jihadharini na nani unayemfanya kuwa rafiki." **(Bihar al-Anwar, Vol. 74, P. 192.)**

Anaenda mbele na kushauri ni namna gani mtu anaweza kuendelea katika mambo yake ya kiroho na kidunia

Mtume (sa) alisema "Kaa pamoja na Muumini tu, na fanyeni chakula chenu kiliwe na watu wema pekee." **(Tirmidhi)**

Hivyo sio vyema kama unajua jukumu lako kukubali kung'ang'ania chochote ambacho ni kizito katika kufikia ndoto zako.

Kijijini kwetu kijana akiweza kutoka kijijini kwenda mjini kwa miezi hata miwili akirudi kutembelea alikuwa anaonekana dhalili kujihusisha na mambo ya kawaida pale kijijini, basi atamaliza muda wake kijiweni akisimulia stori za mjini kwa wenziwe waliowahi kutembelea, nakumbuka kuwa niliweza kutoka kwa ajili ya masomo ya sekondari niliporudi nilikuwa naweza kwenda shamba na kuendelea kuchunga mbuzi, na kuishi sawa na utaratibu wa nyumbani, nilikuwa nabanana na ndugu kunywa uji asubuhi mpaka bibi yangu alikuwa ananiuliza kwani hukui tu, vivyo hivyo likizo zangu za Jamia nilikuwa naenda kuchimba madini na kufanya mambo yangu yaliyokuwa yananifanya nijisikie huru sikutaka kukumbatia marafiki wasio na maono yangu lakini sikuacha kuongea vizuri na kushirikiana nao.

Mtangazaji na mchekeshaji wima wa marekani mwenye asili ya Afrika kusini Trevor Noah katika mahojiano Fulani alitolea mfano wa jambo hili kuwa ni kama kufunga mkanda uwapo safarini katika siti ya gari, ni muhimu sana kufunga mkanda kwani ni salama mno kwa maisha yako, na hata saa nyingine unajisahau kuwa umefunga mkanda lakini unapotaka kukurupuka kuondoka unakurudisha nyuma na kukukumbusha upo, lakini unapotaka kushuka na kuenda kufanya mambo muhimu ni lazima uufungue kwanza kwani usipoufungua utabaki katika sehemu hio hio.

Vivyo hivyo ndivyo yalivyo maisha na kuyafikia malengo fulani ni lazima ujitoe nje ya vizingiti fulani hata kama vilikuwa ni usalama wako wakati Fulani.

Sio kila mtu ana uwezo ndani yake wa kuwa Mcha Mungu au tajiri au Msomi au kwenda mbali katika Nyanja yoyote ya kiroho na kidunia, akitokea mmoja kwenu basi ni juu yenu kumlinda na kumstawisha. Na kama hajielewi ni bora aambiwe kuwa yeye ni mteule wa kuwavusha.

Mtume (sa) ametuelezea vyema sana katika hadithi hii kwamba binadamu anapoumbwa na kukamilika basi vitu hivi huwekwa ndani yake.

Amesema "Kisha (Mwenyezi Mungu) humpelekea Malaika aliyepewa jukumu la kuipulizia roho. Kisha (Malaika) anaamrishwa aandike mambo manne: kuandika riziki (riziki ya mtoto), urefu wa maisha yake, matendo yake, na iwapo atakuwa na furaha au huzuni" **(Sahih Bukhari na Muslim)**

Mambo haya yote ni yale yanayomzunguka binadamu kwa ajili ya kutimiza lengo la kuumbwa kwake, hivyo basi ni kama matumizi ya kufikisha katika malengo makubwa basi inabaki katika uwezo wa binadamu kujitafuta katika ujazo wa juu wa uwezo wake ili aweze kuvipata vyote vilivyoandikwa kwa ajili yake na aweze kuvitumia katika kutimiza lengo la uwepo wake hapa duniani yaani kumuabudu Allah.

# Amri hufuatwa kwanza,

## kisha hufikiriwa baadaye kuwa itafuatwa vipi

*Kutoka uk. 12*

na faida kwa mfano umetoka wapi? Unaenda wapi? Unafanya shuguli gani? N.k. Hadhrat Musleh Maud (r.a) alisema kwamba wazungu hawana tabia za aina hiyo. Kwa hiyo, laghw si kitu kinachowaudhi wengine tu bali kila kitu kisicho na faida yoyote ni lagw pia. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba jambo lolote lisilo na shari au faida kwa wengine pia ni Laghw, basi kila mwaminio anapaswa kuongea yale maneno tu ambayo yana shabaha maalum na yafaa ajiepushe na mambo ya upuuzi.

Kuna mfano mwingine uliotolewa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba safari moja mfagizi mmoja ambaye pia alikuwa akifanya kazi ya kuli akaenda kwa mji naye akawakuta watu wote Waislamu na Wahindu wakiomboleza na kulia sana. Huyu mfagizi akamwuliza mtu sababu yake halafu akaambiwa kwamba Maharaja Ranjit Singh (mfale mmoja wa bara hindi) ameaga dunia na kwa kuwa huyu mfalme alikuwa mwadilifu sana aliyeleta amani na usalama katika nchi yake na akawapa waislamu wengi wizara na shughuli za maana katika ufalme wake. Hivyo kifo chake kikawahuzunisha watu wote. Basi huyu mfagizi alipoambiwa kukihusu kifo hiki akashangaa sana na kusema kwamba mbona mnahuzunika na kulia sana juu ya habari hii. Ikiwa mtu kama baba wangu anaweza kufariki basi huyu mfalme ana umuhimu gani. Kwa kuwa huyu mfagizi alitunzwa na baba wake na kwa ajili ya ukosefu wa elimu yake hakuweza kujua umuhimu wa yule mfalme basi akashangaa kwa huzuni ya watu juu ya kifo cha mfalme. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa akieleza mfano huu na kusema kwamba umuhimu wa kila kitu huwa ni tofauti mbele ya kila mtu. Kwa mfano mtoto akipewa almasi hawezi kujua umuhimu wake. Funzo kwa ajili yetu katika mfano huu ni hili kwamba tujaribu kuishi maisha ya kuwanufaisha watu wote bila ubaguzi, hivi tutaweza kupata umaarufu mzuri katika watu ambao utakuwa njia mojawapo ya mahubiri ya Jumuiya yetu pia.

Baadhi ya watu wanapotoa sadaka ndogo au hata kama hawajafanya chochote hufikiri kwamba wamefanya kazi kubwa sana. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alieleza mfano wao kwa kusema kwamba safari moja mtu fulani akamkaribisha mtu mwingine kwa karamu, na akajaribu kumkaribisha vizuri kulingana na uwezo wake. Mgeni alipomaliza karamu na akakaribia kuondoka mwenye nyumba akamwomba msamaha na akasema kwamba mkewe alikuwa mgonjwa na kwa ajili ya sababu zingine pia hakuweza kumkaribisha vile ilivyo, hivyo amsamehe. Mgeni akasema kuwa nimejua dhamira yako ya kusema hivi. Wewe wataka kusifiwa kwa ukarimu wako lakini sitakusifa hata kidogo kwa kuwa mimi nimekufanyia hisani kwa kutochoma mali yako iliyojaa katika chumba chako cha wageni. Ulipokuwa unaniletea chakula nilipata nafasi mara kwa mara nishike kiberiti na nichome nyumba yako, lakini sikufanya hivyo, basi ihsani ni yangu. Hapo mwenye nyumba akamshukuru zaidi. Basi hii ndiyo hali ya watu wasiotaka kuwatolea watu shukrani. Lakini mwaminio yafaa kuwa mwenye kuwatolea shukrani sana wale watu wanaomfanyia ihsani.

Hadhrat Musleh Maud (r.a) amewanasihi masheikh kwa mfano uliotolewa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Kulikuwa mfalme aliyekuwa anampenda sufii mmoja na alikuwa anamwomba waziri wake kuwa ampelekeee kwake. Huyu waziri alikuwa anajua hali ya huyu sufii lakini baada ya kusisitizwa na mfalme akampeleka kwake. Huyu sufii akasema kwamba bw. Mfalme kuna baraka nyingi ya kuhudumia Dini. Kwa mfano Mfalme Alegzendar alihudumia Dini, hii ndiyo sababu kwamba anajulikana sana katika watu hadi leo. Ilhali Alegzendar akazaliwa kabla ya ujaji wa Dini ya Kiislamu. Basi mfalme alipojua hali hii ya ujahili wa huyu sufii akaanza kumchukia sana. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa ananasihi kwamba ni muhimu kuwa na elimu ya kimsingi ya dunia. Masheikh wanapaswa kuwa na adabu za kukaa katika mikutano na ujuzi wa kimsingi wa elimu za kidunia na habari za dunia pia, ili wanapoulizwa maswali wasiseme chochote bila elimu halafu watu wa dunia wapate athari mbaya. Ni muhimu kuwa, na elimu ya kimsingi ya hiyo mikutano ya kidunia pia.

Kuna mfano mwingine ulioelezwa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba kulikuwa tajiri fulani ambaye alikuwa na vijana wawili, naye aliwagawia mali yake yote. Kijana wake mdogo akachukua mali yake na akaenda nayo katika sehemu ya mbali kisha akapoteza mali yake yote katika mambo ya anasa. Baada ya kupoteza mali yake yote akalazimika kufanya shughuli ya mchungaji. Alipoona kwamba hawezi akaamua kurudi kwa baba yake na kumwomba kazi kama mfanyakazi wa kawaida. Baba akafurahi kwa kumwona kijana wake na akamkaribisha sana na akawaamrisha wafanyakazi wake wachinge ndama aliyenona vizuri kwa furaha ya kupokea kijana wake. Kijana wake wa pili alipoona akakasirika na akamwambia baba kwamba mbona unamkaribisha vizuri ilhali mimi ninakuhudumia kwa muda mrefu na sikupoteza mali yako? Baba akajibu kwamba wewe ulikuwa hujapotea nasi tumefurahi juu ya kurudi kwa ndugu yako kwa kuwa amepatikana baada ya kupotea kwake na amehuishwa baada ya kufa kwake. Ujumbe katika mfano uliotolewa ni huu kwamba Mwenyezi Mungu Husamehe watumishi wake wanaoomba msamaha wa dhambi zao, Hupokea toba zao na Huwarehemu sana. Kwa hiyo tunapowakuta ndugu zetu waliotukosea kwamba wanatuomba msamaha basi tuwasamehe na tuwaombee pia. Hata wale wasioomba msamaha tuwaombee kwamba Mwenyezi Mungu Awasamehe na Atusamehe pia.

Binadamu yafaa kuwa na msimamo mmoja katika maisha yake. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa akisema kwamba kulikuwa mfalme fulani aliyekaribishwa bilingani na akalipenda sana. Huyu mfalme aliposifu biligani mbele ya mtumishi wake, naye mtumishi akaanza kusifu bilingani kupita kiasi kwa kufananisha bilingani na vitu vizuri na kueleza sifa nzuri ya mboga huu. Mfalme aliposikia sifa hizi akaanza kula bilingani katika vyakula kwa wingi. Bilingani huwa na athari ya joto, hiyo athari ilipoanza kumtatiza mfalme, basi akasema kumbe biligani si zuri. Hapo mtumishi huyu huyu akaanza kueleza ubaya wa rangi, sura na shari za biligani mbele ya mfalme. Mtu mmoja kati ya wale waliokuwa wanasikia majira yote akamlaumu huyu mtumishi, na huyu mtumishi akamjibu kwamba mimi ni mtumishi wa mfalme wala si mtumishi wa bilingani. Hii ndiyo hali ya Waislamu wa siku hizi, wanasiasa wao na rai wote wawili hawana msimamo mmoja. Wanapoona kwamba faidi yapatikana upande mmoja huelekea upande huu na wakiona kwamba watafaidika upande ule mwingine basi huelekea kule bila kujali kwamba ukweli uko wapi.

Kuna tukio lengine linalohusiana na uhusiano wa Mungu unaoongezwa na ucha Mungu. Sisi Waahmadiyya hatuwezi kufaulu bila uhuisano wa Mungu unaopatikana na ucha Mungu na Hofu ya Kwepo kwake. Basi kila mmoja wetu anapaswa kutafakari na kupanga njia za kuongeza utawa na uhusiano wa Mungu. Kama uhusiano na watu baadhi ya wakati hunufaisha wanadamu basi Uhusiano wa Mungu utatufaidisha kiasi gani. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa akieleza mfano mmoja kwamba kulikuwa mtu ambaye akaamua kusafiri na kabla ya kutoka akaacha mali yake kwa hakimu wa eneo lake. Huyu mtu aliporudi na akamwendea yule hakimu ili amrudishe mali yake. Lakini huyu hakimu akageuza nia na akakataa kwamba amechukua mali yake na akasema kama umenipa mali yako basi uonyeshe risiti au ithibati ya kunipa mali yako. Huyu mtu baada ya kujibiwa hivi akamwendea mfalme na akamweleza habari yote. Huyu mfalme akamjibu kwamba siwezi nikakusaidia katika mambo ya korti kwa kuwa huna ithibati lakini kama unasema kweli basi usiwe na wasiwasi, mimi nitaondoka na jeshi langu kwa kutembea katika njia za mji, nawe utasimama karibu na huyu hakimu, nitakapopita mbele

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

# Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 6

Bendera 19 zashushwa yapandishwa ya Ahmadiyya



HABARI UK> 10

Jitafute Jitambuwe

# Amri hufuatwa kwanza,

## kisha hufikiriwa baadaye kuwa itafuatwa vipi

⚜ Penye upendo hapahitajiwi dalili.

⚜ Amri hufuatwa kwanza, kisha hufikiriwa baadaye kuwa itafuatwa vipi.

⚜ Akili ya asili ni ile izaliwayo na upendo.

Baada ya kusoma Tashhahud na Surah Al-Fatiha, Hudhur[atba] alisema:

Baadhi ya wakati watu wanaongea Laghw amabayo ni maneno yasiyo na maana na ya upuuzi katika mikutano yao. Maneno hayo baadhi ya wakati huudhi watu wengine au yanakosa maana yoyote yanayopoteza nafasi. Katika Kamusi Laghw maana yake ni maneno yasiyo na maana na ya upuuzi, au kuongea bila kutafakari, au kuongea kama baradhuli. Kurani Tukufu imewazuia waaminio kuongea jambo lolote la upuuzi basi maneno ya aina hii. Hadhrat Musleh Maud (r.a) anaeleza hali hii katika mfano ulioelezwa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] kwamba Mungu Amesema katika Kurani Tukufu:

و اذا مروا باللغو مروا كراما۔


(Al-Furqan 25: 73)

Kwamba mwaminio anapoona anapitia kando na jambo hili. Hadhrat Musleh Maud (r.a) anaeleza kwamba wanawake wanapenda kuongea mambo yasiyo na maana kama vile kuulizana bai ya nguo au madoido n.k. Hata baadhi ya wanaume wanazoea hivi pia. Jambo hili ni laghw na linaacha athari mbaya kwa watu wanaokaa pamoja nao. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa akieleza mfano wa mama mmoja aliyenunua pete nzuri ya dhahabu ili awaonyeshe watu lakini watu hawakuiona pete yake. Hivyo kwa sababu ya fikira hii yule mama akachoma nyumba yake. Watu walipomuuliza kwamb je kuna chochote ambacho hakijaungua katia nyumba yake, hapo mara moja akawaonyesha pete yake. Mama mmoja alipoiona pete yake akasifu, hivyo yule mama akamjibu kwamba laiti ungeisifu pete yangu hapo kabla na nyumba yangu haingeungua. Hadhrat Musleh Maud (r.a) anaeleza kwamba hata wanaume pia wanazoea kuzungumza maneno yasiyo na maana ya aina hiyo. Wanaume huanza kuuliza maswali yasiyo

UK. 11



Muhtasari wa hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] ilitolewa Tarehe 27 Mwezi wa Februari, 2016







## Je, Wajua?

Je wajua kuwa mwanahisabati wa kiislam aitwaye Muhammad ibn musa al khawarizmi ndiye aliyegundua hesabu za algebra na kuzitambulisha kwa watu kupitia kitabu chake kiitwacho al-Kitāb al-mukhtaṣar fī ḥisāb al-jabr wal-muqābala (Kitabu Kinachojumuisha Kuhesabu kwa Kukamilisha na Kusawazisha). Waingereza walipoanza mahusiano na waaarabu, ndipo kitabu hicho kilipoingia katika mikono ya wazungu, na elimu hiyo imetufikia kutokea kwa wazungu.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,500/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com